AGOST 29.



HABARILEO UK 19.

# naji safi masomo

ariLEO
a-
nikakati

i ya
hiyo ipo
wa maji

Mwenge
izindu-
landizi
ulazaji
na
i za
weza na

fikia
a kuwa,

mwanzoni mwa Oktoba, mwaka huu itakuwa imekamilika na huduma kuanza mitaani.

Alitaja baadhi ya maeneo yatakayonufaika na mradi huo kuwa ni pamoja na Talawanda, Mdaula, Vigwaza, Magindu, Visezi, Visakazi, Fukayosi, Masuguru na Mioni ambayo yatafaidika kwa kuweka mabomba ya mradi wa tatu unaondelea mitaani.

Alisema kipaumbele kimewekwa katika taasisi za umma husani shule, makanisa, misikiti na zahanati.

"Niwaombe subra wananchi wakati kazi hii inaendelea kufanyika," alisema.

# bati barabara

ao
kilo-
meta
a
89
wa
eza na
han-

izo,

eza
vango

e
o,

wa

lami," alisema.

Katika hatua nyingine; Chinengo ametoa onyo kali akitaka watu kuacha mara moja, tabia ya kuvamia hifadhi za barabara na kwamba, hatua kali za kisheria zitaendelea kuchukuliwa kwa wananchi wanaokiuka sheria hiyo.

"Wilaya ya Rombo kama ilivyo kwa wilaya nyingi za Mkoa wa Kilimanjaro, kuna changamoto ya ufinyu wa ardhi hivyo wananchi wengi wanavamia maeneo ya hifadhi zetu za barabara. ...Barabara zetu zimevamiwa hivyo nitoe rai kwa wananchi kuacha kuvamia hifadhi zetu kwani hatutasita kuwachukulia hatua," alisema.



wa Kitaifa Zanzibar, wakiangalia
Baraza la Wawakilishi).

# Ulega ataka marekebisho mwongozo wa Mnada wa Pugu

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewaelekeza watendaji wa mifugo wa wizara hiyo, kurekebisha mwongozo wa Mnada wa Pugu uliopo Dar es salaam ili kuruhusu shughuli kuanza saa moja asubuhi badala ya saa tatu asubuhi.

Alisema ujenzi wa eneo hilo la kunyweshea mifugo maji utaanza wiki ijayo kwa kuwa mkandarasi ameshapatikana.

Aidha, alielekeza kuanzia sasa mnada huo uanze kufunguliwa saa 1 asubuhi badala ya saa 3.

Ulega alisema hayo katika ziara yake ya kusikiliza kero za wafanyabiashara wa Mnada wa Kimataifa wa Pugu ukiwemo utaratibu wa utoaji wa huduma katika mnada huo.

Alisema kitendo cha huduma hizo kuanza saa tatu badala ya saa moja asubuhi kinasababisha Watanzania wengi kukosa biashara kwa wale wanaotegemea mazao ya mifugo.

"Shusheni muda hadi saa moja asubuhi, ongeeni na watu benki waanze kutoa huduma kuanzia muda huo. Polisi wapo wana uwezo na uweledi wataimarisha ulinzi. Rais Samia Suluhu, anapenda watu wafanye kazi na kulipa ushuru... Naagiza shusheni muda," alisema Ulega.

Ziara hiyo ilikuwa na lengo la kuangalia utekelezaji wa shughuli mbalimbali sambamba na kukagua ujenzi wa uzio unaozunguka mnada huo na kupokea na kushughulikia kero zinazowakabili wafanyabiashara.

Baadhi ya wafanyabiashara walimueleza Naibu waziri Ulega kuwa, biashara katika mnada huo inaanza saa moja asubuhi, lakini changamoto wanayoipata ni suala la ukatishaji wa ushuru ambapo watumishi wanafungua ofisi saa tatu asubuhi kwa mujibu wa mwongozo wa minada.

Aidha, walisema bado wanakabiliana na kero mbalimbali ikiwemo ya uchakavu wa paa la eneo la kuhifadhia mifugo yao, wakisema wakati wa mvua wanapata shida ya kujikinga wao pamoja na mifugo wanayoihifadhi.

Akifafanua kuhusu baadhi ya changamoto hizo, Ulega alisema kuhusu paa la eneo la kuhifadhia, mkandarasi ameshapatikana na kazi ya kupaua na kurekebisha eneo itaanza mara moja na itafanyika usiku na mchana.

Alisema Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imeshafikisha maji katika mnada huo.

Alisema kilichobaki ni miundombinu ya mabomba na mchakato utakamilika ndani ya wiki moja.

Kuhusu uzio, alisema kazi imeshaanza na akamtaka mkandarasi kuhakikisha ifikapo Septemba 5, mwaka huu, kazi hiyo iwe imekamilika.